**SONGWE REGION CO-OPERATIVE UNION (SORECU) LTD**
**REG. NO. AFF-SNG-MBZ-DC-2023-80**

**KUMB.NA AFF/SNG/MBZ/DC/2023/80/VOL.001/2026** **02/04/2026.**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA MAALUM (MIEZI 3)

Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Songwe (SORECU LTD) kinapenda kuwatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Songwe na Momba kuwa tumetangaza ajira za muda maalumu kwa ajili ya Usimamizi wa makusanyo ya Ufuta kupitia mfumo wa Stakabadhi za ghala, zoezi linalosimamiwa na AMCOS kwa kushirikiana na SORECU LTD.Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:

**1. Operation Meneja / Afisa kazi (Nafasi 2).**

**MAJUKUMU:**

- Kuwasimamia wasimamizi wa Maghala waliopo maghala Makuu
- Kusimamia utoaji wa oda za kubeba mizigo (Ufuta) toka maghala ya vyama vya Msingi Kwenda Maghala Makuu.
- Kuhakikisha AMCOS wanawasilisha taarifa za makusanyo na malipo ya wakulima katika kituo cha malipo kwa wakati.
- Kuhakikisha anatoa usaidizi kwa makatibu wa AMCOS namna ya kutumia Mizani ya Kidijitali.
- Kutekeleza majukumu mengine yote atakayopatiwa na mwajiri.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi.
- Uwezo mzuri wa mawasiliano na kufanya kazi na jamii.
- Aliye na uzoefu wa kufanya kazi za Stakabadhi ghalani: aliye na cheti cha WRRB atapewa kipaumbele.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa uadilifu na nidhamu.

Songwe Region Co-operative Union (SORECU) Ltd. Uhuru Street, Vwawa. S.L.P 148, Mbozi - Songwe
Barua pepe: sorecultd@gmail.com

Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

- Kusimamia upokeaji, uhifadhi na utoaji wa mazao maghalani.
- Kutoa usaidizi kwa viongozi wa AMCOS wanaopeleka mazao ghalani katika kujaza taarifa za msingi.
- Kuhakikisha usalama wa mazao na mali zilizopo ghalani.
- Kuweka kumbukumbu sahihi za mazao yanayoingia na kutoka.
- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa hali ya ghala na bidhaa.
- Kuwasilisha ripoti ya ghalani kila siku kwa meneja kazi (Operesheni meneja) wake kila siku jioni.
- Kutekeleza majukumu yote atakayopangiwa na mwajiri wake.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi.
- Uzoefu wa kazi za ghala au uhifadhi (Cheti cha WRRB atapewa kipaumbele).
- Uadilifu na umakini katika utunzaji wa kumbukumbu.

**3. Mtunza Stoo (Nafasi 1).**

**MAJUKUMU:**

- Kusimamia stoo na vifaa vyote vya chama.
- Kurekodi vifaa vinavyoingia na kutoka stoo.
- Kuhakikisha usafi na mpangilio mzuri wa stoo.
- Kufanya hesabu za mara kwa mara za vifaa vilivyopo.
- Kutoa ripoti ya vifaa vinavyoingia na kutoka kwa meneja shughuli.
- Kutekeleza majukumu yote atakayopangiwa na mwajiri wake.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi.
- Ujuzi wa msingi wa utunzaji wa stoo.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa umakini na nidhamu.

**4. Karani / Wasimamizi wa Vituo vya Malipo ya Wakulima (Nafasi 4)**

**MAJUKUMU:**

- Kusimamia malipo ya wakulima kwa usahihi na kwa wakati.
- Kuweka kumbukumbu za kifedha na kufanya upatanisho wa hesabu.
- Kutoa taarifa za mapato na matumizi ya vituo vya malipo.



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

- Kuhakikisha taratibu za kifedha zinafuatwa ipasavyo.
- Kuwasaidia viongozi wa AMCOS kuandaa taarifa za malipo ya wakulima wao.
- Kusaidia kutatua changamoto za wakulima wanaofika katika kituo cha malipo.
- Kusaidia kutoa elimu ya uandishi wa vitabu kwa viongozi wa AMCOS.
- Kutekeleza majukumu yote atakayopangiwa na mwajiri wake.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi.
- Ujuzi wa hesabu.
- Ni lazima awe na uwezo wa kutumua kompyuta (MS Word na MS Excel).
- Uaminifu na uwajibikaji mkubwa katika kushughulikia fedha.

**5. Wakala wa Fedha (Nafasi 1).**
**MAJUKUMU:**

- Kusimamia miamala ya kifedha kwa kutumia mifumo ya kidigitali.
- Kutoa huduma za kifedha kwa wanachama na wakulima.
- Kuhakikisha usalama wa fedha na taarifa za miamala.
- Kutoa taarifa za kila siku za miamala iliyofanyika.
- Kuandaa taarifa ya kila mwezi.
- Kufanya majukumu mengine yote atakayopangiwa na mwajiri wake.

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Elimu ya Kidato cha Nne au zaidi.
- Uzoefu au ujuzi wa huduma za kifedha au uwakala.
- Uaminifu na uwezo wa kutumia teknolojia za malipo.

**SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.**

- Mwombaji awe na elimu ya kuanzia Kidato cha Nne au zaidi.
- Mwombaji awe na uadilifu, uwajibikaji na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea.
- Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika mazingira ya vijijini.
- Mwombaji awe na uwezo mzuri wa mawasiliano na ushirikiano.



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

- Uzoefu katika kazi husika utakuwa ni faida ya ziada.
- Mwombaji awe na umri wa miaka 18-45
- Mwombaji awe mkazi wa eneo la Wilaya linapopatikana ghala kuu la kuhifadhia Ufuta.
- Walio ndani ya Kijiji/Kata linapopatikana ghala kuu watapewa kipaumbele
- Mwombaji awe na kitambulisho cha Nida, Mpiga kura au leseni ya udereva.
- Mwombaji awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- Ni lazima mwombaji awe na uwezo wa kutumia kompyuta kwa vipengere vya M/S Word na M/S Excel.

**JINSI YA KUOMBA.**

Waombajwote wanatakiwa kutuma maombi yao yakijumuisha:

- Barua ya maombi
- Wasifu binafsi (CV)
- Nakala za vyeti vya taaluma
- Barua ya utambulisho (ipitishwe kwa Afisa kilimo kata na Mtendaji wa kijiji).
- Nakala ya kitambulisho

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:

**Meneja Mkuu**
**Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Songwe**
**S.L.P 148,**
**Mbozi-Songwe.**

Kupitia barua pepe: **sorecultd@gmail.com**
Maombi yatakayowasilishwa kwa njia tofauti hayatapokelewa.
Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 10 Aprili 2026.

Imetolewa na .

SONGWE REGION COOPERATIVE UNION LIMITED
02 APR 2026
AFF-SNG-MBZ-DC-2023-80
P.O.BOX 148, MBOZI-SONGWE

.........................................................
DAUDI ANDREW SLAHHI
MENEJA MKUU



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

**NAKALA.**

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika,
Mkoa wa Songwe,
S.L.P 23,
**MBOZI - SONGWE.**

Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi,
Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Songwe,
S.L.P 148,
**MBOZI - SONGWE.**



Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/